Afasia ni nini?

Swahili



Labda unmewahi kukabiliwa na afasia mara ya kwanza muda uliopita. Hapo mwanzo afasia huleta maswala kama; afasia ni nini, huenea vipi na shida gani zingine huweza kuibuka?

Afasia ni nini?

Kila binadamu hutumia lugha. Kusema, kupata maneno yafaayo, kuelewa, kusoma, kuandika na kuonyesha vitendo ni sehemu ya utumiaji wa lugha. Kama baada ya dhara ya ubongo mojawapo ya vipengele vya lugha vinapo kosa kufanya kazi, hii huitwa afasia. Kwa hivyo afasia – A (=kukosa) phasia (=kusema) humaanisha kuwa mtu hawezi kusema jambo ambalo angetaka kusema. Yeye hawezi kutumia lugha tena. Bali na afasia, kulemaa hutokea na shida kulingana na:

- kuigiza kwa ufahamu
- kuangalia mazingira
- kuweka makini, kujitolea, na kikumbuko

Watu hawawezi kufanya mambo mawili kwa wakati mmoja tena

Watu wengi hukasirika wakati wanapokwenda ng'ambo kwa likizo na wasiweze kusema vyema kile wanachomaanisha, au kutokuelewa vyema kile ambacho mwenzao anasema. Hata katika nchi ambazo tunafahamu lugha hiyo vyema, tunaweza kupitia jambo hili kwa mfano tunapo mwendea daktari. Katika nchi ambazo hatuifahamu lugha vyema, kuongea kwetu na wenyeji huwa imeadimika na saa zote hatuwezi kuitisha chakula ambacho tunanuiya kuila sana. Watu wanaougua afasia hupitia shida hizi saa zote. Hakuna watu wawili wanaougua kutokana na afasia ambao wako sawa: afasia ni tofauti kwa kila mtu. Uzito na eneo wa afasia hutegemea, kati ya mambo mengine, eneo na uzito wa tata la ubongo, ustadi wa lugha mbeleni, na ubinafsi wa mtu. Watu wengine wanaougua afasia wanaweza kuelewa lugha vyema, lakini huwa na shida ya kupata maneno mwafaka au kutunga sentensi. Kwa upande mwingine wengine huongea sana, lakini kile wanachosema hakiwezi au ni kigumu kueleweka kwa mwenziwe.; watu hawa kwa kawaida huwa na shida kuelewa lugha. Ujuzi wa lugha wa watu ambao wanaugua kutokana na afasia ni kati ya mambo haya mawili. Unapaswa kujua ya kwamba: mtu anayeugua kutokana na afasia kwa kawaida huwa na uerevu wake timamu!. Kwa kawaida huwa kunatokea uponyevu wa ghafla wa lugha hiyo wakati ugonjwa wa afasia unapokuwa. Uponyevu huu huwa sio wa kabisa. Kwa kufanya mazoezi, bidii na ushupavu, endeleo unaweza kutokea.

Ukuzi wa afasia

Afasia huwa kutokana na dhara ya bongo. Chanzo cha dhara hiyo ya ubongo kwa kawaida huwa ni tata katika mshipa wa damu. Tata hilo pia hujulikana kama pindo la mshipa,kuvuja kwa mshipa. Katika maneno ya utabibu inajulikana kama CVA: Cerebral (=ubongo) Vascular (=mshipa) Accident (=ajali). Mambo mengine yanayosababisha kukuwa kwa afasia

ni kama kuumia (kuumia kwa ubongo kutokana na kwa mfano (barabara) ajali au kidonda kwenye ubongo
Bongo zetu huhitaji oksijeni na sukari ili kufanya kazi. Kwa hivyo baada ya CVA au ueneaji wa damu katika ubongo kutatanishwa, chembe chembe za ubongo hufa katika sehemu hiyo. Ubongo huwa na sehemu tofauti tofauti ambazo hufanya kazi mbali mbali. Kwa watu wengi sehemu za lugha hupatikana kwenye upande wa kushoto wa ubongo. Kama kuna ajali katika sehemu hizi la lugha basi tunaongea kuhusu afasia.

Shida gani zingine hutokea?
Ni vigumu kuwa mtu anaweza kugonjeka kutokana na afasia pekee. Kwa kawaida sehemu zingine za ubongo huwa zimeadhirika. Mfano mojawapo ya shida zingine ambazo hutokea ni kama:

- Hali ya *hemiplegic* (hemi=nusu, plegic=kipooza). Kwa watu wanaougua kutokana na afasia mara nyingi huwa ni upande wa kulia katika mwili. Kufanya kazi kwa misuli katika pande moja mwilini huwa imeadhirika, na hii husababisha kutokuwa na uhusiano kwenye misuli.

- Kupotea kwa nguvu ya kuona (hemianopsia, hemi=nusu, opsia=ona). Kwa kawaida watu huweza kuona kila kitu ambacho kiko katika upande nusu ulio na afya, lakini sio katika upande huo mwingine ulio na madhara.

- Kutojua jinsi vitendo fulani vinapaswa kutendwa (apraxia, a=hapana, praxia=kitendo). Vitendo rahisi kama kuvaa nguo, kula na kunywa haviwezi kutendwa kwa fahamu tena. Mtu anaye ugua kutokana na apraxia hawezi, kwa mfano, kujua kuzima mshumaa anapoagizwa kufanya hivyo (kitendo cha fahamu), lakini anaweza kuzima kiberiti ambayo anakishika wakati anafikiri kuwa vidole vyake vitaungua.
- Shida kula, kunywa na kumeza (dysphagia, dys=sio vyema, phagia=kumeza). Kwasababu ya tata ya ubongo misuli za digrastiki na misuli za kumeza hufa, kuwa na hisia nyingi au hata bila hisia. Hii husababisha kula na kunywa kuwa ngumu. Kwasababu ya kupooza au ukosefu wa hisia katika sehemu ya shavu, mate huweza kuzoa kwenye upande wa mdomo bila kujua.
- Shida ya kukumbuka. Wakati wa kukumbuka jambo, lugha huwa na umuhimu. Kwasababu ya shida za lugha kikumbuko huwa hakifanyi kazi vizuri. Kwa hivyo ni muhimu kuandika maneno muhimu; hii humwezesha mtu anayeugua kutokana na afasia kukumbuka mambo.
- Kupokea mambo tofauti. Saa zingine watu hupokea tofauti kwa mambo baada ya pindo la mshipa kushinda hapo mbeleni. Uwezo wa kuonyasha hisia huwa ngumu. Kuna uwezekano kuwa mtu anaweza kucheka na kulia saa zote. Pia kuna uwezekano kuwa inaweza kumchukua muda mrefu kuwacha kufanya hivyo.
- Ugonjwa wa kifafa. Ubongo unapopona kutokana na jeraha kovu huwa kwenye bongo. Wakati mwingine kovu hii huleta shida ya saketi ya umeme kwenye ubongo. Kutokana na hiyo, mwili hushikwa na kifafa, mtu huwa na shida ya kupunga hewa, na yeye

anaweza kuzirahi. Kitendo hiki cha kifafa huweza kuchua dakika chache, lakini kwa kawaida huanza mara tu na uoga wa mtu anayeipitia na familia yake vilevile huwa kubwa.

Mambo haya yaliyo na shida zingine hayana mwisho. Ishara za ugonjwa wa afasia na /matokeo huwa tofauti kulingana na kila mtu binafsi. Kila shida ambayo imetajwa hapo juu inaweza kutokea kwenye afasia lakini sio za lazima.

Tiba ya afasia

Watu wengi wanaougua kutokana na afasia wamelazwa hospitalini kwa muda Fulani. Kulazwa huko mara nyingi hutokana baada ya dhara ya unbongo. Baada ya kutoka hospitalini watu wengi ambao wanaugua kutokana na afasia huhitaji tiba zaidi. Sio dhahiri ni nani wanayeweza kumwendea ili waweze kupata usaidizi. Tafadhali mwendee daktari wako ili aweze kukuelekeza. Tiba ya afasia kwa kawaida huwa inawachiwa wataalamu wanaojulikana kama warudishaji wa usemi. Mtu anayeugua kutokana na afasia anapaswa kupata urudishaji wa usemi. Muda wa kutibiwa huwa inalingana na kuponya kutokana na afasia na pia masharti ya nchi unamoishi.

Masharti *ya mawasiliano*

Kwasababu ya afasia jinsi ambayo mtu huelewa jambo au kujieleza hugeuka. Kwa kutumia vyema vipengele vya mawasiliano vilivyosalia watu huweza kuwasiliana na mtu anayeugua kutokana na afasia. Mtu ambaye anayo afasia ya hali ya juu* huwa anaweza kuelewa maneno muhimu katika sentensi. Yeye huelewa maneno fulani. Kelewa mambo kutokana na maneno fulani inaweza kusababisha kutokuelewana, kwa maana kushikanisha maneno fulani na kujua vitu fulani maneno huweza kutoeleweka. Wakati mwingine sisi na mtu anayeugua kutokana na afasia hufikiri kuwa tumefahamiana. Jibu lingine baadaye linaonyesha kuwa hatukuelewana.

Kama ungelitaka kumwambia mtu aliye na afasia jambo

- Kwanza, chukua muda wako kwa mawasiliano. Kaa chini vizuri na umwangalie machoni
- Kama unatumahi kuwa na mawasiliano, basi sema jambo rahisi kujihusu na baadaye uliza maswali ambayo unafahamu majibu wewe mwenyewe
- Zungumza pole pole na pia utumie sentensi fupi, na uweke sisitizo kwenye maneno ya muhimu kwenye sentensi
- Andika maneno yalio ya muhimu zaidi. Rudia maneno na umpe muuguzi wa afasia kile ulichoandika. Muuguzi huyo wa afasia anaweza kukitumia kama ukumbusho ama kama njia ya mawasiliano
- Msaidie mtu anayeugua kutokana na afasia kwa shida zake wakati anapojaribu kijieleza kwa kuonyeshea kidole, kuonyesha vitendo, kuchora, au kuandika na kumuuliza kama yeye anaweza kuonyeshea kidole, konyesha vitendo, kuchora au kuandika kitu kutokana nacho. Tafuta pamoja kwenye kamusi au kitabu cha mawasiliano.

Kama mtu anayeugua kutokana na afasia anataka kukuambia jambo
Kwanza inapaswa kuwa dhahiri ni nani anahusika, nini itatendeka au kilitenedeka na pengine wapi au wakati gani jambo hilo litafanyika au lilifanyika. Ni muhimu uulize swali mwafaka, uwe mbunifu na uendelee kwa njia mwafaka iwezekanayo. Jaribu kuuliza maswali yalio na majibu ya kuchagua, ambapo utaweka majibu yanayoweza kuchaguliwa kando kando

Vifaa vya mawasiliano

Katika nchi nyingi kuna vitabu maalam vya kuonyesha kidola kwenye picha ambavyo vina maneno na michoro kwa kuonyeshea kidole kwenye maneno au picha mtu anaweza kufafanua vyema kile anacho maanisha. Mwone daktari wako au warudishaji wa semi kama vifaa hivi viko kwenye nchi yako. Kama haviko, unaweza kuunda kitabu cha mawasiliano mwenyewe. Ndani yake unaweza kuweka picha au michoro na maneno yalio muhimu kwa mtu anaye ugua kutokana na afasia. Kwa njia hii gumzo kuhusu mambo yanayofanyika inaweza kufanyika na hisia zinaweza kuzungumziwa.

Wakati tunawasiliana na mtu anayeugua kutokana na afasia, kwa kutumia kitabu kilicho na picha ya kuonyeshea kidole unaweza kujaribu pamoja kuangalia mambo muhimu ya kuwasiliana kuhusu. Hakikisha kuwa unayo kalamu na karatasi mkononi. Baadaye unaweza kuandika yale maneno yalio ya muhimu kwenye mawasiliano chini ya wenziwe, ili iwe rahisi kufuata na kukumbuka vipengele vya mawasiliano hayo.

Uvumilivu huweza yote

Kuwa na mazungumzo na mtu ambaye anugua kutokana na afasia huhitaji masaa mengi na uvumilifu. Kando na mambo yalio tajwa hapo juu kunawezekano kuwa bado hamuelewani. Tulia kidogo halafu ujaribu baadaye, utafaulu vyema!

Maelezo zaidi
Katika tovuti ya Shirikisho la Kimataifa la Afasia unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu afasia katika lugha mbali www.aphasia-international.com. Humo utapata mwelekeo katika shirika zingine ambazo zitakupa maelezo kuhusu afasia katika lugha zao.

Nia ya tovuti hii ni kubainisha afasia na kunuisha msingi wa vikundi vya watu wanaougua, ili kuzuia watu wanaougua kutokana na afasia kuwa katika upweke.